Mpendwa Mzazi/Mlezi

**Juu: Sensa ya Maendeleo ya Awali ya Australia**

Barua hii na Karatasi ya Ukweli iliyoambatishwa ni pamoja na taarifa muhimu kuhusu Sensa ya Maendeleo ya Awali ya Australia (Australian Early Development Census (AEDC)) na utunzaji unaopendekezwa wa taarifa za kibinafsi za mtoto/watoto wako.

Shule yetu itashirikia katika AEDC kati ya Mei na Julai mwaka huu. AEDC ni sensa ya kitaifa ambayo hufanywa kila baada ya miaka mitatu na Serikali ya Australia, kwa ushirikiano na serikali za majimbo na wilaya. Inapima jinsi watoto wanavyokua wakati wa kuanza mwaka wao wa kwanza wa shule ya kila siku.

AEDC ni ya hiari na haipimi jinsi watoto wanavyofanya vizuri shuleni, wala jinsi shule yao inavyolinganishwa na shule nyingine. Badala yake, inaonyesha jinsi watoto wanavyokua na kuendelea katika maeneo matano muhimu, ni nini kinafanywa vizuri na kinachoweza kuboreshwa. Data za AEDC hutumiwa na shule, mashirika ya utoto wa awali, watafiti na serikali ili kuwasaidia kupanga na kuboresha huduma na usaidizi kwa watoto na familia. Hivyo ndivyo kwani ni muhimu kwa watoto wote wa mwaka wao wa kwanza kujumuishwa katika AEDC. Waweza kujifunza zaidi juu ya jinsi data za AEDC hutumika kwa https://www.aedc.gov.au/

**Je, ina maana gani kwa mtoto wako?**

AEDC hukamilishwa na walimu kulingana na ujuzi wao wa watoto. Watoto hawahitaji kufanya chochote ili kujumuishwa katika sensa na watahudhuria masomo kama kawaida wakati sensa inapofanyika.

Sensa itaanza kwa tarehe inayofuata: ____________________

Walimu watajibu maswali kuhusu maeneo matano muhimu ya ukuaji wa awali wa utotoni, ambayo ni: afya ya kimwili na ustawi, ukomavu wa kihisia, uwezo wa kijamii, ujuzi wa lugha na utambuzi (msingi wa shule), na ujuzi wa mawasiliano na ujuzi wa jumla. Unaweza kusoma maswali yote kwa https://www.aedc.gov.au/avedi

**Unaweza kuwa na uhakika kwamba faragha ya mtoto wako italindwa.**

Tunaelewa jinsi ilivyo muhimu kuweka taarifa za mtoto wako kuwa ya faragha. Hii ndiyo sababu AEDC hutumia tovuti salama kukusanya na kuhifadhi taarifa zake.

Maelezo zaidi kuhusu jinsi data za AEDC (ikiwa ni pamoja na maelezo ya mtoto wako) inavyokusanywa, kulindwa na kutumiwa yamo kwenye Karatasi ya Ukweli.

**Je, wazazi wanahitaji kufanya nini?**

Kwa madhumuni ya AEDC, Idara ya Elimu ya Serikali ya Australia inaomba idhini yako ya kukusanya taarifa za kibinafsi kuhusu mtoto wako kutoka shuleni kwetu. Hii ni pamoja na taarifa inayojulikana kuhusu afya ya mtoto wako.

Ikiwa unakubali kukusanywa wa taarifa za mtoto wako, huna haja ya kufanya yoyote.

Usipokubali kukusanywa kwa taarifa za mtoto wako, tafadhali wasiliana na mtu aliyeorodheshwa hapa chini kabla ya tarehe iliyoonyeshwa hapa chini na taarifa kuhusu mtoto wako haitakusanywa:

Jina la mtu wa kuwasiliana naye ____________________

Maelezo ya mawasiliano ya mtu wa kuwasiliana naye shuleni ____________________

Tarehe ya mwisho kuwasiliana na mtu huyo wa shule ili kujiondoa ____________________

Unaweza pia kuondoa idhini yako baada ya muda huu. Ukifanya hivyo, basi Idara ya Elimu ya Serikali ya Australia itaacha kutumia taarifa za mtoto wako na haitatoa kwa mtu mwingine yeyote. Hata hivyo, taarifa ambazo tayari zimeshirikiwa, kuripotiwa au kuchapishwa hayiziwezi kuondolewa na zinaweza kuendelea kutumika (lakini mtoto wako hatatambulishwa kibinafsi katika taarifa hizo).

Ili kujua zaidi kuhusu AEDC, tafadhali soma sehemu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara kwenye tovuti ya AEDC kwa https://www.aedc.gov.au/parents/faq-for-parents au piga simu 1800 092 548.

Taarifa za mtoto wako zitatumika tu kwa madhumuni yaliyofafanuliwa katika barua hii na katika Karatasi ya Ukweli. Taarifa ya Faragha iliyo kwenye tovuti ya AEDC inatoa maelezo zaidi kuhusu jinsi taarifa zake zitalindwa na kushirikiwa, na yanaweza kupatikana katika: www.aedc.gov.au/parents/privacy-statement

Asante kwa kuunga mkono na AEDC.

Mkuu wa shule

**Huduma ya mkalimani wa simu**

Ikiwa unahitaji usaidizi wa mkalimani ili kuwasiliana na shule, tafadhali piga simu 131 450, mwambie opereta ni lugha gani unayohitaji na umwombe apige simu shuleni. Opereta atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia kwa mazungumzo yako. Hutatozwa kwa huduma hii.